**TAARIFA YA MGODI WA KIWIRA KWA MKUU WA MKOA WA SONGWE MHE. BRIGEDIA JENERALI NICODEMAS ELIAS MWANGELA MKUU WA MKOA WA SONGWE KWENYE ZIARA MGODINI TAREHE 19 SEPTEMBA 2018**

Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa,

Kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Madini la Taifa(STAMICO), na wafanyakazi wote, ninayo heshima kubwa kukukaribisha wewe mwenyewe na msafara wako kutembelea mgodi wetu siku ya leo.

**UTANGULIZI**

Taarifa hii ya mgodi inazingatia maeneo makuu matatu, yaani historia fupi ya migodi ya Kiwira na Kabulo, shughuli zinazoendelea kwa sasa na mwisho matarajio ya mbeleni.

## 1.0 HISTORIA YA KIWIRA NA KABULO

### 1.1 Kiwira

Mgodi huu ulianza kwa msaada wa Serikali ya China mwaka 1988 ukiwa na tani million 14.64 za makaa ya mawe zinazoweza kuvunwa kwa faida. Mpaka shughuli za uzalishaji zinasimama mwaka 2008 zaidi ya tani milioni 2 zimeshachimbwa.

Kati ya , 1988 na , 2005 mgodi ulikuwa unamilikiwa na Serikali kupitia STAMICO kwa asilimia 100 wakati huo mgodi ulikuwa unazalisha umeme wa Megawati 6 na kuusambaza Wilaya za Tukuyu na Kyela. Kuanzia 2005 hadi 2012 umiliki wa mgodi ulikuwa chini ya ubia kati ya Serikali [30%] na TanPower Resources Limited [70%]; hii ni baada ya Serikali kubinafsisha mgodi kutokana na sera zilizokuwepo wakati huo . Mbia alipewa kuendesha mgodi huu kwa lengo la kuanzisha kituo kipya cha umeme cha Megawati 200, kupanua uzalishaji mgodini na kujenga njia mpya ya umeme hadi Mwakibete - Mbeya. Hata hivyo mbia alishindwa kupata mtaji wa kutekeleza lengo hilo na hivyo kushindwa kuendelea na mgodi. Uzalishaji ulisimama kabisa ilipofika mwaka 2008. Aidha Julai 1, 2012 Serikali kwa makubaliano na mbia mwenzake iliuchukua umiliki

wa mgodi na hatimaye kuurudisha tena kwa STAMICO mwaka 2014 ili iuendeleze.

## 1.2 Kabulo

Leseni ya utafiti (Prospecting License) ya makaa yam awe Kabulo pia nayo inamilikiwa na Serikali kupitia STAMICO.Utafiti wa awali wa wataalam wa British Mining Consultancy Limited (BMCL) uliofanyika katika miaka ya1970 na 1980 unaonesha kuwa kuna zaidi ya tani milioni 35 na eneo lina ukubwa wa kilometa za mraba 33.84 na uvunaji wake unaweza kuwa wa juu, *open pit*.

# 2.0 SHUGHULI ZINAZOENDELEA KWA SASA

## 2.1 Kabulo

Kwa upande wa Kabulo shughuli za uzalishaji wa majaribio zilianza mwishoni mwa mwezi Aprili 2017 na mpaka kufikia sasa zaidi ya tani 8,000 zimekwishachimbwa. Wateja wetu wakuu wmekuwa ni kampuni za saruji za hapa nchini na wengine kutoka Kenya. Mpaka sasa makaa ya mawe jumla ya tani 3,987.4 zimeuzwa , kati ya hizo, tani 1,380 zimeuzwa nje ya nchi.

Katika kuboresha na kuongeza nguvu shughuli za uchimbaji, Shirika limetafuta na kupata mkandarasi wa uchimbaji, CMG Construction Ltd. Mkandarasi huyu amepewa mkataba wa kuzalisha tani 700 kwa siku kwa muda wa miezi sita. Mkandarasi huyo tayari alikabidhiwa eneo la uchimbaji tarehe 10 Septemba, 2018 na kwa sasa yupo katika kukamilisha usafirishaji wa mitambo(mobilization) kuja mgodini na kuanza kazi mara moja.

## 2.2 Kinu cha kusaga Makaa ya Mawe

Katika kuboresha ubora wa makaa ya mawe na kuongeza wigo wa wateja, STAMICO kwa kutumia mafundi wake waliopo mgodini, walianza kazi ya kufufua kinu cha kusaga makaa yam awe kilichoacha kufanya kazi mwaka 2008. Kazi hiyo ilianzamwezi Mei 14, 2018 na ilikamilika ndani ya miezi miwili. Kwa sasa kazi zinazoendelea ni

majaribio ya kinu hicho na marekebisho madogo madogo kadri yanavyojitokeza katika majaribio ya mitambo.

## 2.3 Mgodi wa chini Kiwira

Mgodi wa chini, pia upo katika maandalizi ya ukarabati, kazi hii itaanza kulingana na mahitaji na ukubwa wa soko, hasa baada ya uzalishaji wa makaa ya mawe Kabulo kuanza.

## 2.4 Uzalishaji wa Nishati Mbadala – Coal Briquettes

Mipango mingine ni pamoja na kuanzisha uzalishaji wa nishati mbadala ya briquettes kwa kutumia makaa ya mawe na kusambaza teknolojia ya uzalishaji huo kwa wajasiriamali nchini. Lengo ni Mkoa mama na nchi nzima kupambana na ukataji miti kwa ajili ya nishati majumbani na kwenye taasisi badala yake watumie nishati hii mbadala. Itakumbukwa kuwa briquette hutengenezwa kutokana na mabaki ya makaa ya mawe.

## 2.5 Changamoto

Changamoto kubwa katika utekelezaji wa mradi huu ni urefu wa barabara itakayotumika kutoka mgodini Kabulo hadi Kiwira kupitia Kasumulu - Kyela kwa ajili ya kuleta makaa hayo kiwandani kwa lengo la kuyaongezea ubora. Barabara hii ina urefu wa kilomita 36. Kilomita 16 kati ya hizo ni barabara ambayo haina uwezo wa kupitisha magari makubwa yenye uzito wa zaidi ya tani 15. Urefu huu wa barabara unaongeza gharama za uzalishaji na hivyo kuufanya mradi usiweza kujiendesha kwa faida.

Changamoto hii inaweza kutatuliwa kwa kufungua barabara ya zamani ambayo ina urefu wa kilomita takribani 7 toka Kiwira hadi Kabulo kupitia mto Mwalisi. Barabara hii iliacha kutumika baada ya daraja la mto Mwalisi kusombwa na maji mwaka 2002.

Hatua za kufufua barabara hiyo tayari zimeanza kupitia Mkuu wa Wilaya ya Ileje na TARURA Wilaya. Tunatoa shukrani kubwa kwa Mkuu wa Wilaya ya Ileje, Mbunge wa jimbo la Ileje pamoja na TARURA

Wilaya kwa juhudi zao  za kuhakikisha kuwa barabara hii inafufuliwa tena ili iweze kusaidia sio shughuli za uchimbaji makaa ya mawe Kabulo tu bali pia kuwasaidia wananchi wanaozunguka maeneo inakopita barabara hiyo.

Aidha  Mgodi unakabiliwa na changamoto ya mtaji kwa ajili ya shughuli za uchimbaji wa makaa yam awe.

## 3.0 MATAZAMIO YA MBELENI

a) Kuunganisha Mradi wa Kabulo na Kiwira kwa kuitengeneza upya barabara ya zamani inayounganisha Kabulo na Kiwira kupitia mto Mwalisi yenye urefu wa kilometa 7;
b) Kufufua uzalishaji wa  umeme katika kituo cha zamani cha Megawati 6;
c) Kufufua  na kuanza uzalishaji wa makaa ya mawe underground – Kiwira;
d) Kuanzisha kituo cha kufundishia uzalishaji wa Nishati Mbadala katika eneo la mgodi wa Kiwira;
e) Kuanzisha kituo kipya cha umeme cha Megawati kati ya 200 na 600 na  kujenga njia mpya ya umeme kati ya Kiwira na Mbeya.

## 4.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa, kwa kuwa mradi huu una tija si katika mkoa wako tu bali Taifa kwa ujumla, tunaomba uwezeshe matengenezo ya barabara ya kuunganisha mgodi wa Kabulo na Kiwira ili uzalishaji wa makaa ya mawe uweze kuanza mara moja. Msaada wako katika jambo hili unahitajika kwa kiasi kikubwa na ndio utakaowezesha mgodi kujiendesha kwa mafanikio.

Asanteni sana kwa kunisikiliza.